

# Una haki ya kupata maelezo kuhusu “Kadirio la Nia Njema” yanayofafanua gharama ya huduma yako ya afya

Kwa mujibu wa sheria, watoa huduma za afya wanahitaji kuwapa wagonjwa wasio na aina fulani za bima za afya au ambao hawatumii aina fulani za bima za afya, kadirio la bili ya bidhaa na huduma za afya kabla ya bidhaa au huduma hizo kutolewa.

- Una haki ya kupewa maelezo kuhusu Kadirio la Njia Njema (Good Faith Estimate) kwa bidhaa au huduma zozote za afya ukiomba, au wakati unapanga kupokea huduma au bidhaa hizo. Gharama hizi ni pamoja na bili zinazohusiana kama vile vipimo vya matibabu, dawa za kuagizwa, vifaa na ada za hospitali.
- Ukipanga kupokea bidhaa au huduma ya afya angalau siku tatu za kazi kabla, hakikisha kuwa mtoa huduma wako au kituo cha afya kinakupa maelezo yaliyoandikwa kuhusu Kadirio la Njia Njema ndani ya siku moja ya kazi baada ya kupanga. Ukipanga kupokea bidhaa au huduma ya afya angalau siku 10 za kazi kabla, hakikisha kuwa mtoa huduma wako au kituo cha afya kinakupa maelezo yaliyoandikwa ya Kadirio la Njia Njema ndani ya siku tatu za kazi baada ya kupanga. Unaweza pia kumwambia mtoa huduma au kituo chochote cha afya kikupe maelezo ya Kadirio la Njia Njema kabla ya kupanga kupokea bidhaa au huduma ya afya. Ukifanya hivyo, hakikisha kuwa mtoa huduma au kituo cha afya kinakupa maelezo yaliyoandikwa kuhusu Kadirio la Njia Njema ndani ya siku tatu za kazi baada ya kuomba.
- Ukipokea bili kutoka kwa mtoa huduma au kituo chochote cha afya inayozidi Kadirio la Njia Njema kwa angalau \$400, unaweza kupinga bili hiyo.
- Hakikisha kuwa unahifadhi nakala au picha ya hati ya Kadirio la Njia Njema na ya bili hiyo.

Ukiwa na maswali au ukitaka maelezo zaidi kuhusu haki yako ya kupata hati ya Kadirio la Njia Njema, tembelea [cms.gov/nosurprises/consumers](https://cms.gov/nosurprises/consumers), tuma barua pepe kwa [FederalIPPDRQuestions@cms.hhs.gov](mailto:FederalIPPDRQuestions@cms.hhs.gov), au piga simu kwa **800.985.3059**.

Ili upate orodha kamili, tafadhali omba brosha kutoka kwa mtoa huduma wako wa afya au utembelee [corewellhealth.org/policies](https://corewellhealth.org/policies)

